Tumfahamu Yesu—#5

Mahali Maalumu Pa Yesu



PATAKATIFU (HEKALU)

Baada ya Mungu kuwapa Amri zake Kumi wana wa Israeli, alitaka kuongea na Musa. Mungu akamwambia Musa, "Panda huku mlimani" (Kutoka 24:12). Kwa hiyo Musa akapanda mlimani kwenye njia yenye mwinuko mkali wa mlima. Juu ya mlima Mungu alikuwa ndani ya wingu zito, jeusi; na hapo alizungumza na Musa.

Mungu alimwambia Musa kwamba aliwapenda sana Waisraeli kiasi kwamba alitaka kuishi nao. Walikuwa wakiishi katika mahema madogo madogo na Mungu alihitaji hema maalum ili aweze kuishi kando yao. Inashangaza kiasi gani!

Kwa siku 40 Mungu alizungumza na Musa mlimani. Mungu alimwambia Musa jinsi ya kutengeneza hema lake. Hema la Mungu la pekee litaitwa Patakatifu. Mungu alihitaji Musa alitengeneze ili watu wajue kuhusu Patakatifu pake pa mbinguni. Lazima ijengwe kwa uangalifu sana. Lakini Musa angepata wapi vifaa vya kujengea Patakatifu?

Wakati wa usiku Waisraeli waliondoka Misri, Wamisri waliwapa dhahabu, fedha, shaba nyeupe nyingi sana, na nguo zenye rangi zinazong'aa, na vitu vingine vya thamani. Kwa hiyo Mungu alimwambia Musa akusanye sadaka kwa ajili kujengea Patakatifu kutoka kwa wana wa Israeli. Mungu akasema, "Chukua sadaka yangu kwa yeyote anayetoa kwa hiari katika moyo wake" (Kutoka 25:2). Mungu alihitaji zawadi kutoka kwa wale tu waliotoa kwa furaha na moyo wa ukarimu.

Wana wa Israeli walikuwa tayari kutoa kwa furaha. Walitoa vitu vingi

sana hadi Musa alipowambia waache kutoa!

Mungu alichagua watu wawili maalum kuisimamia kazi ya ujenzi wa Patakatifu, na Mungu "aliwajaza ujuzi wa kufanya kazi za kila aina" (Kutoka 35:35).



Sean Eichelberger

Mungu pia alimchagua Haruni na wana wake kufanya kazi katika Patakatifu pake. Waliitwa makuhani na walikuwa wakimwakilisha Yesu, ambaye sasa ni Kuhani wetu Mkuu mbinguni.

Ilichukua miezi sita kujenga patakatifu; na kazi ilipokamilika, kila kitu kilikuwa kama vile Mungu alivyokuwa amempa maelekezo Musa jinsi ya kupatengeneza. Mungu akapendezwa, "na utukufu wa Bwana ukapajaza Patakatifu" (Kutoka 40:34).

Picha iliyopo hapo juu inaonyesha jinsi Patakatifu pa Mungu pa kupendeza jinsi palivyoonekana.

TAFAKARI...

- **Je, Mungu anapenda kuwa karibu nasi, kama alivyopenda kuwa karibu na wana wa Israeli?**
- **Je, Mungu anapenda tutoe kwa moyo wa furaha?**
- **Mungu aliwasaidia watu kujenga patakatifu. Atatusaidia kufanya chochote anachohitaji tufanye?**
- **Je, Yesu anataka kutusaidia? Soma Waebrania 4:14–16**

(UA WA PATAKATIFU) BEHEWA

Ukuta uliozunguka patakatifu ulikuwa pazia jeupe. Kulikuwa na mlango mmoja tu ambao watu wangepita wanapoingia kwenye behewa. Pazia jeupe lilimwakilisha Yesu, ambaye kamwe hajawahi kutenda dhambi.

Kitu cha kwanza katika behewa kilikuwa ni madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa. Ilitengenezwa kwa shaba nyeupe. Kila asubuhi na jioni mwanakondoo mkamilifu alitolewa kama sadaka juu ya madhabahu hii. Mwanakondoo aliwakilisha Yesu aliyekufa kwa ajili ya dhambi zetu.

Karibu na mlango wa Patakatifu kulikuwa na birika. Lilikuwa ni bakuli kubwa lililotengenezwa kwa vioo vinavyong'aa vilivyokuwa vimetolewa na wanawake. Maji safi na angavu yaliwekwa ndani ya birika ili makuhani waoshe mikono na miguu yao kabla ya kuingia katika Patakatifu pa Mungu. Maji yaliwakilisha Yesu anayeweza kuosha dhambi zetu.

PATAKATIFU

Patakatifu palikuwa mahali maalum ndani ya behewa. Pia kulikuwa na mlango mmoja tu wa kuingia ndani yake. Mlango huo ulimwakilisha Yesu. Yesu alisema, "Mimi ni mlango" (Yohana 10:9). Yesu ni njia pekee ya msamaha na kuingia mbinguni.

Mlango wa patakatifu na dari vilitengenezwa kwa vitambaa za rangi ya bluu, zambarau, na nyekundu zikiwa zimefumwa maumbo ya malaika wa kupendeza. Kuta za Patakatifu zilitengenezwa kwa nguzo na mbao

iliyofunikwa na dhahabu inayong'aa.

Ndani ya patakatifu kulikuwa na vyumba viwili; kimoja kiliitwa Patakatifu na kingine Patakatifu pa Patakatifu. Pazia zito zuri liliwekwa katikati ya vyumba vile viwili.

PATAKATIFU PA KWANZA

Katika Patakatifu kulikuwa na vitu vya aina tatu na vyote vilikuwa vimefunikwa kwa dhahabu. Upande wa kushoto mwa chumba kulikuwa na kinara cha taa chenye taa saba zilizokuwa zikiwaka na kutoa mwanga unaong'aa sana. Nuru ile ilimwakilisha Yesu, aliyesema, "Mimi ni nuru ya ulimwengu" (Yohana 8:12).

Upande wa kulia wa chumba kulikuwa na meza ya mikate ya wonyesho. Juu yake kulikuwa na mikate kumi na mbili iliyokuwa imefunikwa kwa uvumba. Mikate ilimwakilisha Yesu, aliesema, "Mimi ndimi mkate wa uzima" (Yohana 6:35).

Katikati, mbele ya pazia zito, zuri, kulikuwa na madhabahu ya uvumba. Mungu mwenyewe aliwasha moto katika madhabahu hii. Kila

All images on this spread: Sean Eichelberger

TAFAKARI...

- **Kila kitu hekaluni kiliwasaidia Waisraeli kujifunza kuhusu Yesu. Je, unaweza kukumbuka baadhi ya vitu hivyo ni vitu gani?**
- **Amri Kumi zilihifadhiwa wapi?**
- **Je, Mungu anaweza kutubadilisha, na kutusaidia kutii sheri yake, Amri Kumi?**
- **Mwanakondoo alimwakilisha nani? Je, unashukuru kwamba Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zetu?**

asubuhi na jioni kuhani alifanya na kuchoma uvumba juu yake. Uvumba uliwakilisha wema wa Yesu. Tunapoomba Yesu anawafunika wema maombi yetu na wema wake na kuyapeleka juu kwa Mungu Baba.

Sean Eichelberger

PATAKATIFU PA PILI

Ndani ya patakatifu pa pili kulikuwa ni sanduku la agano, kifaa kilichokuwa cha muhimu sana. Lilikuwa ni sanduku lililochongwa vizuri sana na kufunikwa kwa dhahabu. Juu yake kulikuwa na kifuniko maalum kilichoitwa Kiti cha Rehema. Juu yake kulikuwa na malaika wawili wa dhahabu wakiangalia chini ile Kiti cha Rehema.

Katikati ya malaika wa dhahabu wawili kulikuwa na nuru iliyong'aa sana iliyoitwa Shekina. Ilikuwepo mahali hapo.

Ndani ya sanduku la agano chini ya Shekina nzuri kulikuwa na vipande viwili vya mawe bapa. Juu ya mawe kulikuwa na maneno yenye Amri Kumi. Mungu alikuwa ameyaandika kwa kidole chake mwenyewe.

Mara moja kwa mwaka, kuhani mkuu, aliyemwakilisha Yesu, aliingia

Patakatifu pa pili kuomba kwa ajili ya watu.

KUONDOA DHAMBI

Hema takatifu ya Mungu inatuonyesha jinsi Mungu anavyotusamehe dhambi na kutusaidia tusiendelee kufanya dhambi. Mwisraeli alipofanya dhambi, alileta mwanakondoo mkamilifu kwenye madhabahu iliyokuwa ndani ya behewa. Kumbuka, mwanakondoo alimwakilisha Yesu, "Mwanakondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu" (Yohana 1:29).

Mdhambi aliweka mikono yake juu ya kichwa cha mwanakondoo na kuungama dhambi yake halisi. Kisha alimwuua mwanakondoo asiye na hatia. Hii inaonyesha jinsi dhambi zetu zilivyomwuumiza Yesu alipokufa msalabani. Dhambi inaumiza, sana sana, sivyo?

Yesu peke yake anaweza kusamehe dhambi zetu na kuziondoa. Yesu peke yake anaweza kutusaidia tusiendelee kufanya dhambi na kutusaidia tuwe watii. Ni kiasi gani Yesu anatupenda!

Fungu la Biblia la kujifunza

"Na wanifanyie patakatifu nipate kukaa kati yao." Kutoka 25:8

Nachagua

Je, unahitaji kumwomba Yesu akusamehe dhambi zako na akusaidie kuwa mtii?

Ombi langu

Mpendwa Mungu, asante kwa kunipenda sana. Asante kwa sababu Yesu alikufa ili kuniondolea dhambi zangu. Tafadhali naomba unisamehe dhambi zangu zote na unisaidie kukutii. Katika jina la Yesu, amina.

My Bible First © 2016
www.mybiblefirst.org
Fungu zote za Biblia zinatoka Union Version.

Front cover photo: © Richard Taylor
License—http://creativecommons.org/licenses/by/2.0/

SOMO KUTOKA ASILI

Unawaona wanyama wangapi katika picha hapa chini? Wawili! Hawa ni wanyama wa aina gani? Wanaitwa kangaroo. Je, unaweza kuwaona vizuri? Hapana. Picha inaonyesha vivuli vyao tu.

Fikiria kama ungekuwa hujawahi kumwona kangaroo hapo awali. Ungejifunza kiasi gani kuhusu kangaroo kwa kuwaangalia kwenye picha? Je, miguu yao ya mbele inalingana na miguu yao ya nyuma? Je, masikio yao ni makubwa au madogo? Shingo yake ni ndefu au fupi? Je, mkia wake ni mwembamba au mnene?

Tunaweza kujifunza mengi kwa kuangalia kivuli. Lakini, je, kivuli kinatuambia kila kitu kinachotokea kwenye picha? Hapana. Je, unafikiri kangaroo wanatazama kwenye machweo ya jua? Au wanamwangalia mtu anayewapiga picha? Hatuwezi kujua. Je, kangaroo hawa wana manyoya mekundu au manyoya kijivu? Na, je, mikia yao ni mirefu kiasi gani? Picha haituonyeshi, sivyo?

Katika somo hili la Biblia, tulijifunza kuwa Mungu alitaka Waisraeli wamjue zaidi Yesu na mpango wake wa ajabu wa kutuokoa. Lakini Waisraeli hawakuweza kumwangalia Yesu moja kwa moja. Kwa hiyo Mungu alimwambia Musa jinsi ya kujenga Patakatifu. Palikuwa na vifaa vya aina mbalimbali na sikukuu za aina mbali mbali. Kila moja iliwasaidia Waisraeli wajue jambo fulani kuhusu Yesu. Tunaweza kusema zilikuwa kama “vivuli” vya Yesu.

Je, vitu hivyo katika patakatifu viliwaeleza kila kitu kuhusu Yesu? Hapana. Vivuli havituambii kila kitu. Lakini bado Mungu alitaka Waisraeli wajifunze kwa kadri ilivyowezekana. Biblia inasema kwamba mambo haya yalikuwa ni “kivuli cha mambo yajayo, bali mwili ni wa Kristo” (Wakolosai 2:17).

Hatuna hema tena; lakini kutokana na Biblia isemavyo kuhusiana nayo, bado tunaweza kujifunza mengi kuhusu Yesu na mpango wake wa kutuokoa kutoka dhambi zetu. Je, unapenda kuendelea kujifunza zaidi kuhusu Yesu kutoka Biblia?

Photo © Chris Samuel; License—http://creativecommons.org/licenses/by/2.0/